

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI KUHUSU JINA LA SHULE YA SEKONDARI MWALIMU NYANGE

02 Januari, 2025.

Hivi karibuni kumekuwa na mijadala na mitazamo tofauti kwenye mitandao ya kijamii na maeneo mingine kuhusu Jina la Shule mpya ya Sekondari iliyojengwa katika Kata ya Tandika kupewa jina la **'Mwalimu Nyange'** ambalo ni Jina la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Ifahamike kuwa, Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani haijapokea barua yeyote ya maoni, mapendekezo au malalamiko kutoka kwa mwananchi yeyote kupinga Jina la shule hiyo ya Sekondari.

Hata hivyo ieleweke kuwa, shule hiyo mpya ya Sekondari kupewa Jina la **Mwalimu Nyange** ni mapendekezo yaliyotolewa na wananchi wa mitaa mitano (5) ya Kata ya Tandika ambayo ni **Mtaa wa Shule ya Msingi Majengo, Tandika, Mmingano, Liyawile na Mtawike** katika Mikutano ya wananchi wote wa Mitaa hiyo na baadaye kupitishwa na kuridhiwa na Kikao Cha Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Tandika (WDC) kilichofanyika **tarehe 05/09/2024** ambacho ndicho chombo chenye Mamlaka ya kupendekeza jina la Shule katika hatua za awali za usajili.

Aidha baada ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kupokea mapendekezo hayo yaliyoambatishwa na Muhtasari wa Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) iliyafanyia kazi na kupelekwa ngazi za juu kwa ajili ya kuendelea na taratibu za usajili wa Shule hiyo.

Hata hivyo, kutokana na uwepo wa mijadala na mitazamo mbalimbali juu ya suala hilo, Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara-Mikindani imerudisha suala hilo kwenye Ofisi ya Kata ya Tandika ili lijadiliwe upya kwa kuwashirikisha tena wananchi wa mitaa yote ya Kata ya Tandika kama ilivyofanyika hapo awali na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Manispaa mapendekezo ya jina litakalokuwa limepitishwa na wananchi na kuridhiwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) ili liweze kupelekwa ngazi husika kwa utekelezaji.

R.H Maiga

KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA

MTWARA-MIKINDANI.